Swali: Katika Mathayo 5:14 biblia inasema kuwa *“Nuru yetu na iangaze mbele za Watu”*, halafu tukienda kwenye Mathayo 6:1 maandiko yanasema *“tusifanye wema wetu machoni pa watu”*, hapa nahitaji ufafanuzi.

---

Jibu: Tusome

> *Mathayo 5:14 “Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima.*
>
> *15 Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani.*
>
> *16 VIVYO HIVYO NURU YENU NA IANGAZE MBELE YA WATU, WAPATE KUYAONA MATENDO YENU MEMA, WAMTUKUZE BABA YENU ALIYE MBINGUNI”.*

Tusome pia Mathayo 6:1-2..

> *Mathayo 6:1 “Angalieni msifanye wema wenu machoni pa watu, KUSUDI MTAZAMWE NA WAO; kwa maana mkifanya kama hayo, hampati thawabu kwa Baba yenu aliye mbinguni.*
>
> *2 Basi wewe utoapo sadaka, usipige panda mbele yako, kama wanafiki wafanyavyo katika masinagogi na njiani, ILI WATUKUZWE NA WATU”*

Mistari hiyo miwili haijichanganyi, isipokuwa fahamu zetu ndizo zinazojichanganya.

Bwana Yesu aliposema Nuru yetu na iangaze mbele za watu.. ni ili Mungu atukuzwe kupitia matendo yetu mema tunayoyafanya!… Lakini tukifanya jambo lolote ambalo halitamrudishia Mungu utukufu bali litatupa sisi utukufu, huo sio wema Bwana Yesu alioumaanisha kuwa tuungaze..Ndio maana hapo kwenye *Mathayo 5:16 anamalizia kwa kusema.. “wapate kuyaona matendo yenu mema, WAMTUKUZE BABA YENU ALIYE MBINGUNI.*”..Na sio watutukuze sisi!!!.

Lakini tunapofanya Wema huku lengo letu ni watu watupe sisi utukufu, au watusifu, au watuone ni mashuhuri, huo sio wema

bali ni Ubaya uliovaa vazi la wema ndani yake.. ndio maana katika huo mstari wa 2, Bwana anaweka msisitizo kwa kusema…

> *Mathayo 6:2 “Basi wewe utoapo sadaka, usipige panda mbele yako, kama wanafiki wafanyavyo katika masinagogi na njiani, ILI WATUKUZWE NA WATU”.*

Umeona hapo lengo la wao kufanya mema yote hayo ni ili watukuzwe na watu, na si Mungu atukuzwe kupitia wao!..Hivyo hiyo ni dhambi!..

Jambo lolote tulifanyalo lisilomrudishia Mungu utukufu hata kama liwe jema kiasi gani, mbele za Mungu ni dhambi!.

Wakati Fulani Mfalme Herode aliwafanyia Wema watu wa Tiro kwa kuwasamehe na kuwapatia riziki, na akaandaa hotuba ambayo iliwafurahisha sana watu wa Tiro, hata kufikia hatua watu hao kumtukuza kwa kusema “Sauti yake ni sauti ya Mungu na si mwanadamu!”..

Na utaona baada ya pale, Mungu alimpiga Herode kwa Chango,

kwasababu hakumpa Mungu utukufu, bali alijitukuza yeye!..*(Habari hiyo unaweza kuisoma katika kitabu cha Matendo 12:20-24)*.

Kwahiyo na sisi hatuna budi kuzipima dhamira zetu katika wema wote tunaoufanya.. Je! Lengo letu ni kumpa Mungu utukufu, au kujitukuza sisi. Kama wema tunaoufanya ni kwa lengo la Mungu kutukuzwa basi huo tuufanye kwa bidii sana kwasababu mwisho wake ni Mungu kutukuzwa, lakini kama lengo ni sisi kutukuzwa, basi tujihadhari na huo.

Maran atha!

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii
>> https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10[1]

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:
Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

---

Mada Nyinginezo:

NGAZI 7 AMBAZO MKRISTO NI LAZIMA AZIPANDE KUUFIKIA UKAMILIFU.[2]

LAKINI NINYI, NDUGU, MSIKATE TAMAA KATIKA KUTENDA MEMA.[3]

NI SAA KUMI NA MBILI (12) TU, ZA KRISTO KWAKO.[4]

Ibada ni nini,Na je ili ikamilike inapaswa iwe na nini na nini?[5]

IFAHAMU HUZUNI NA FURAHA YA MALAIKA.[6]

Rudi nyumbani[7]

Share on:
WhatsApp
Endnotes:

1. https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10: https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10

2. NGAZI 7 AMBAZO MKRISTO NI LAZIMA AZIPANDE KUUFIKIA UKAMILIFU.: https://wingulamashahidi.org/2021/03/10/ngazi-7-ambazo-mkristo-ni-lazima-azipande-kuufikia-ukamilifu/
3. LAKINI NINYI, NDUGU, MSIKATE TAMAA KATIKA KUTENDA MEMA.: https://wingulamashahidi.org/2021/03/16/lakini-ninyi-ndugu-msikate-tamaa-katika-kutenda-mema/
4. NI SAA KUMI NA MBILI (12) TU, ZA KRISTO KWAKO.: https://wingulamashahidi.org/2020/12/14/ni-saa-kumi-na-mbili-12-tu-za-kristo-kwako/
5. Ibada ni nini,Na je ili ikamilike inapaswa iwe na nini na nini?: https://wingulamashahidi.org/2020/09/11/ibada-ni-ninina-je-ili-ikamilike-inapaswa-iwe-na-nini-na-nini/
6. IFAHAMU HUZUNI NA FURAHA YA MALAIKA.: https://wingulamashahidi.org/2020/12/30/ifahamu-huzuni-na-furaha-ya-malaika/
7. Rudi nyumbani: https://wingulamashahidi.org